


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA WAKUSANYA USHURU

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbanga anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi ya Ajira ya Muda (Vibarua) kwa nafasi ya Wakusanya Ushuru - Nafasi 40

1. SIFA ZA MWOMBAJI

Awe Mtanzania mkazi wa Halmashauri ya Mji Mbanga.

Awe na umri sio chini ya miaka 18 au zaidi ya miaka 55.

Awe na Elimu ya Darasa la Saba na kuendelea.

Awe Muadilifu, Mwaminifu na hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai.

Awe na uzoefu wa kutumia “**Smart – Phone**” EFD katika miamala ya malipo.

2. KAZI/MAJUKUMU

Kukusanya Ushuru wa Ukusanyaji taka, Madini ya Ujenzi, Stendi, Vyoo, Misitu, Machinjio, Vibali vya Ujenzi, Maegesho na/au kadiri atakavyopangiwa na Afisa Mapato wa Halmashauri ya Mji Mbanga. Mwombaji aeleze sifa na uzoefu wake kwenye kazi ya ukusanyaji mapato.

3. MASHARTI YA JUMLA

- Barua ya Maombi iambatanishwe na barua ya Utambulisho kutoka Ofisi ya Mtendaji wa Mtaa anaishi mwombaji, pia aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, vyeti vya elimu, picha moja”Passport Size” na barua ya mdhamini kwenda kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji, mwenye mali isiyohamishika ndani ya Halmashauri ya Mji wa Mbanga iliyopitishwa na Mtendaji wa Mtaa anaishi Mdhamini.
- Mwombaji ataje Mtaa na Kata anayoishi.

4. MALIPO

Kazi ni Mkataba wa Miezi mitatu(3) ambayo malipo yatazingatia Sheria ya Ajira Cap 300”**Wages Order**”2013 na/au Asilimia ya Makusanyo.

Barua za maombi ziletwe kwa mkono ifikapo au kabla ya tarehe 23/01/2025 saa 9:30 Alasiri kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi wa Mji, S.L.P 135, **MBINGA**

Dkt. Kung'e K. Nyamuryekung'e

KAIMU MKURUGENZI

HALMASHAURI YA MJI

MBINGA

**MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI
MBINGA**